TANESCO SACCOS

Suluhisho la Mtaji

MREJESHO WA MKUTANO MKUU WA CHAMA ULIOFANYIKA OKTOBA 2022

CHAMA CHA USHIRIKA WA AKIBA NA MIKOPO TANESCO

CHAMA CHA USHIRIKA WA AKIBA NA MIKOPO TANESCO

UANDIKISHWAJI

TANESCO SACCOS iliandikishwa Mei 9, mwaka 1968 na kupewa namba ya usajili 1843. TANESCO SACCOS ni Chama kilichosajiliwa na TUME YA MAENDELEO YA USHIRIKA na kupewa leseni namba TCDC.022.0001.2018 kwa mujibu wa sheria ya ushirika Na. 6 ya mwaka 2013.

DIRA

Kuwa SACCOS inayoongoza Afrika Mashariki kwa huduma bora za fedha na zinazokidhi mahitaji.

DHAMIRA

i. Kujenga mifumo imara na endelelevu ya ukusanyaji akiba, hisa na amana.
ii. Kukuza ujumuishi wa huduma za kifedha kwa wanachama wa wasio wanachama kupitia bidhaa na huduma nafuu.
iii. Kukuza usawa wa kijinsia na ushiriki wa vijana kupitia fursa sawa.
iv. Kujenga uwezo na uelewa wa wanachama kupitia elimu na mafunzo.

TUNU ZA TANESCO SACCOS

Tunu ni misingi inayoongoza TANESCO SACCOS katika utendaji kazi na namna inavyohusiana na wadau wake: Tunu hizo ni huduma bora na kumjali mteja, ubunifu na uvumbuzi, weledi, ushirikiano na utawala bora.

CHAMA CHA USHIRIKA WA AKIBA NA MIKOPO TANESCO

KUTOKA KWA: MWENYEKITI **KUM: TS/AGM/2023/01**	**KWENDA KWA: WANACHAMA WOTE** **TAREHE : 28.02.2023**

YAH: MIKUTANO YA MREJESHO NA TAARIFA KWA WANACHAMA MATAWINI

Chama kinawatangazia Wanachama wote kuwa, kinatarajia kuanza kufanya Mikutano ya Mrejesho wa Mkutano Mkuu wa mwaka 2022 katika matawi yake nchi nzima kuanzia tarehe 18.03.2023 ili kuwajulisha juu ya maamuzi yaliyofikiwa na kuwapatia taarifa mbalimbali za maendeleo ya Chama. Agenda za Mkutano:

1. Taarifa: Dondoo na Majibu
2. Hesabu za Chama kuishia Disemba 2021
3. Maazimio ya Mkutano Mkuu wa mwaka 2022
4. Taarifa kuhusu Huduma za Mikopo
5. Uchaguzi wa Wawakilishi - Matawini
6. Usajili wa Wanachama katika mfumo wa FOSA mobile - USSD

Ofisi ya Chama inapenda kuwajulisha wanachama kuwa:

1. Mwanachama atajisajili katika rejesta ya mahudhurio na rejesta hiyo itafungwa na Mwenyekiti wa Mkutano dakika 45 baada ya Mkutano kuanza.

2. Wanachama wote waliohudhuria kikao, watasaini mara 2 (check in & Check out) ili kuwa na akidi halali wakati wote wa Mkutano.

NB:

1. Bajeti ya maandalizi itumwe kwa Meneja wa Chama.
2. Posho italipwa kwa wanachama waliohudhuria kikao tu (sitting allowance).

Andrea Hilary
Katibu wa Bodi

1.0 UTANGULIZI

Chama cha Ushirika wa Akiba na Mikopo TANESCO kinapenda kuwakaribisha wanachama wote katika Mkutano wa kupokea dondoo (maoni) kwa ajili ya kuwasilishwa katika Mkutano Mkuu wa mwaka 2022 kwa majadiliano na maamuzi. Sambamba na maoni hayo kupokelewa, Uongozi wa Chama unapenda kutumia nafasi hii kutoa elimu kwa wanachama kuhusu bidhaa mpya kwa wanachama na taarifa kuhusu msuala yanayotekelezwa na Chama.

2.0 TAARIFA: DONDOO NA MAJIBU

Na.	DONDOO	MKOA	MAJIBU
1	Posho za vikao ziongezwe mpaka kufikiaTshs. 150,000	Kibaha/Kahama/Dodoma&Kondoa/Geita/Kibondo/Mtera/Mafia/Lindi/Kidatu&Kilombero/Kilimanjaro/Iringa/Masasi/Mtwara/Musoma/Songea/Mwanza/Singida/Newala/Loliondo/Temeke/Lushoto/Chalinze&Mlandizi/Morogoro/Tanga/Bagamoyo/Kilindi/Same/Mbeya/Kinondoni kaskazini.	Chama hakitoweza kuongeza posho ya kikao kutokana na vipaumbele vilivyowekwa kwa mwaka 2023, ikiwa ni kukuza ukwasi na utendaji wa Chama.
2	Chama kiongeze kiwango cha mkopo wa Boresha Maisha kutoka Tshs. 30,000,000 mpaka Tshs 100,000,000	Kibaha / Geita /Kidatu & Kilombero / Ifakara- / Kihansi / Musoma / Newala / Tanga / Bagamoyo / Same / Ilala/Mbeya/Songwe	Chama kitaboresha viwango vya mikopo kulingana na hali ya ukwasi.
3	Chama kiboreshe mfumo wake wa Mobile APP kwa kuongeza huduma kwenye mfumo wa IoS.	Kahama / Iringa / Karatu Kiteto / Kondoa / Lushoto / Bagamoyo	Lipo katika utekelezaji wa mwaka 2022.
4	Riba ya mkopo wa maendeleo na Boresha Maisha zipunguzwe mpaka kufikia 9% kwa mwaka.	Kahama / Kibondo / Pangani / Kilimanjaro / Musoma / Manyara / Kidatu / Njombe / Ilala / Shinyanga / ETDCO / Mwanza / Loliondo / Temeke	Maboresho yanayohusisha riba yatazingatiwa wakati wa mapitio ya sera 2023
5	Tozo za kuangalia salio kupitia TANESCO SACCOS Mobile APP.	Nzega & Igunga / Dodoma / ETDCO / Bagamoyo	Tozo hizi zinahusisha gharama za wabia wanaosaidia kutoa huduma. (kampuni za simu)
6	Kiwango cha mkopo wa dharura kiongezwe kutoka Tshs 3,000,000/= mpaka Tshs 6,000,000/= ma marejesho yafanyike kwa miezi 24.	Dodoma / Geita / Pangani / Kilimanjaro / Masasi / Loliondo / Bagamoyo / Mbeya / Songwe/ Kinondoni kaskazini	Chama kitaboresha viwango vya mikopo kulingana na hali ya ukwasi.

Na.	DONDOO	MKOA	MAJIBU
7	Chama kiongeze thamani ya hisa moja kutoka Tshs 5,000/= mpaka Tshs 7,000/= kwa kila hisa na kiwango cha chini kuchangia kiwe Tshs 20,000/= kwa mwezi.	ETDCO / Ilala / Mtwara / Kilimanjaro	Chama katika Mpango Mkakati wa 2024-2028 kitazingatia kuongezwa umiliki wa hisa kwa kila mwanachama.
8	Utaratibu uliopo katika mkopo wa Usafiri wa kuweka rehani chombo hicho uondolewe.	Geita / Mwanza/Iringa/Mafia	Dhamana ya mkopo ni matakwa ya sera na utaratibu wa mikopo.
9	Mkopo wa Ujasiriamali uongezwe kiwango hadi milioni 20 na muda wa marejesho kutoka miezi 24 ya sasa hadi miezi 36.	Geita / Mwanza / Loliondo/Lindi/Masasi	Chama kitaboresha viwango vya mikopo kulingana na hali ya ukwasi.
10	Mkopo wa Maendeleo utolewe kwa kufuata utaratibu wa kuzidisha mara 5 ya akiba za mwanachama, na muda wa marejesho uongezeke na kuwa miezi 72.	Kibondo / Manyara / Kidatu& Kilombero / Ifakara / Simanjiro / Arusha / Chalinze / Morogoro / Mbeya / Songwe / Ilala	Chama kitaboresha viwango vya mikopo kulingana na hali ya ukwasi.
11	Chama kiboreshe huduma za mobile APP kwa kuwezesha mikopo ya papo kwa papo, elimu na dharura iombwe kupitia Mobile APP.	JNHPP / Mtera / Musoma / Ilala / Geita / Singida	Chama kinatafiti uwezekano wa kuanza huduma za papo kwa papo kwa kupitia mobile APP.
12	Chama kiongeze wigo wa kununua madeni kutoka taasisi nyingine za fedha kwa kuanza kulipia deni lisilozidi Tshs. 25,000,000 badala Tshs 15,000,000 ya sasa.	Lindi / Newala / Mtwara	Chama kitazingatia hali ya ukwasi katika kununua madeni ya wanachama kutoka taasisi nyingine za fedha.Kwa sasa ni milioni 15.
13	Kiwango cha michango kwa wanachama kiwe Tshs 100,000 kutoka Tshs 65,000/= kama ilivyopendekezwa na kwa wanachama wenza- kiwe Tshs 50,000 kwa mwezi.	Lindi / Mbeya / Mtwara / Kinondoni kaskazini/Loliondo	Uongozi unapendekeza kiwango cha chini kuchangia kuwa Tshs. 100,000

Na.	DONDOO	MKOA	MAJIBU
14	Chama kiboreshe sera zake kwa kuruhusu Mwana-chama aliyekopa mkopo wa Boresha Maisha akope baada ya kurejesha 1/3 ya mkopo wa awali badala ya 1/2 ya awali.	Kidatu & Kilombero / Ifakara / Kihansi / Nyumba ya Mungu / Kilindi / Same	Maboresho yanayohusisha sera yatazingatiwa wakati wa mapitio ya sera 2023
15	Chama kianzishe ushirikiano na Benki ya NMB ili kuwezesha Wanachama kupata huduma pale ambapo Benki ya TCB haipo.	Kidatu & Kilombero / Mtwara	Chama kinaboresha upatikanaji wa huduma kwa VISA cards sambamba na uwepo wa Mobile App Chama hakiwezi kuwa na ubia na benki Zaidi ya moja kwa akaunti moja.
16	Mkopo wa Elimu utumike kununua mikopo ya wanachama waliosomeshwa na *loan board.*	Kihansi	Mkopo wa Maendeleo na Boresha inaweza kulipa deni la *Loan Board.*
17	Chama kiongeze aina za bima kwani wanachama wengi wanamiliki majengo na biashara	Kilimanjaro	Limepokelewa kwa utekelezaji
18	Gharama za ATM card za visa zipungue kutoa 25,000/= hadi 15,000/=	Kilimanjaro/Mafia/Lushoto/Songea	Hizi ni gharama za benki mbia kwa *card za VISA.*
19	Chama kiongeze bidhaa zake kwa kufungua akaunti za kuweka pesa kwa muda maalumu (fixed deposit)	Kilimanjaro	Lipokelewa, Chama kinawakaribisha wanachama kuweka amana katika akaunti ya Fixed (Riba inayotolewa ni asilimia kati ya 3 hadi 5)
20	Ili kuhamasisha wastaafu kuendela kuwa wanachama hata baada ya kumaliza muda wake wa utumishi, Chama kiruhusu wastaafu kuweza kuchukua mpaka 80% imuwezeshe kuendelea kuwa mwanachama.	Iringa/Tanga/Kinondoni South	Mstaafu anaruhusiwa kupunguza 50% ya michango yake baada ya kustaafu.

Na.	DONDOO	MKOA	MAJIBU
21	Ili kupunguza gharama za uendeshaji wa shughuli za Chama,Chama kiangalie uwezekano wa kutuma makabrasha ya vikao kwa njia ya emails ili kupunguza gharama za uchapishaji.	Iringa/Mbeya/Mtera	Limepokelewa kwa utekelezaji kwa majaribio katika mikoa hii. Tutapima ufanisi wake.
22	Ili kurahisisha zoezi la Mfanyakazi kupitisha mshahara wake Fosa, Chama kiangalie uwezekano wa kumuomba mwajiri aiandikie barua taasisi ya kibenki aliyokuwepo mwanachama.	Iringa/Mtera/Tabora/Kinondoni South	Linatekelezwa na maafisa rasilimali watu wa Shirika. Mwanachama aende kuomba huduma hiyo.
23	Chama kiongeze muda *(maturity date)* wa kupunguza akiba kwa Mwanachama na kuwa kipindi cha mwezi mmoja badala ya siku 21 za sasa.	Tarime/Tunduru	Chama kinatarajia kuondoa utaratibu wa kupunguza akiba, ili kukuza ukwasi wa Chama na kuweza kuwahudumia mikopo kwa wakati.
24	Chama kianzishe huduma ya *Credit Card* kwa Wanachama wake.	Arusha/Temeke	Limepokelewa kwa utafiti.
25	Chama kiwawezeshe wanachama wake kutoa fedha kupitia madirisha ya benki ya TCB.	Chalinze	Limepokelewa kwa utekelezaji katika mwaka wa fedha 2023
26	Katika hatua ya kupunguza matumizi, Chama kiangalie uwezekano wa kupunguza idadi ya wajumbe wa Mkutano mkuu	Morogoro	Uongozi umefanya tathmini ya idadi ya wawakilishi iliyopo, na kujiridhisha ni stahimilivu kwa Chama na inaakisi uwakilishi wa wanachama katika matawi.
27	Chama kiboreshe Masharti yake kwa kuweka kipengele cha ulazima wa kupitisha mshahara kwa njia ya akaunti ya FOSA kuwa lazima.	Karatu/Iringa	Chama kitaendelea kuhamasisha wanachama kuhamia FOSA kwa hiyari ili kufaidi huduma za FOSA

Na.	DONDOO	MKOA	MAJIBU
28	Kila mwanachama anayetaka kugombea nafasi ya ujumbe wa Bodi aweke akiba ya angalau kiasi cha fedha cha Tshs 6,000,000	Karatu	Chama kinatarajia kuboresha vigezo vya kugombea Uongozi (Bodi/Kamati ya Usimamizi) kuwa na akiba angalau Tshs. milioni 12 Na Mwakilishi Tshs. milioni 5.
29	Chama kiboreshe Huduma ya mawasiliano *(Customer Service)*, Taarifa na Simu zote ziwe zinahifadhiwa (Record).	Tanga / Kilimanjaro	Limepokelewa kwa utekelezaji.
30	Kwa mwanachama anayepitisha mshahara wake kupitia akaunti ya FOSA, aruhusiwe kuwasilisha maombi yake bila kuambatanisha salary slip kwa kuwa taarifa za makato kwenye akaunti zinaonekana kwenye akaunti hiyo.	Kilindi	Hati ya mshahara (Payslip) ni muhimu kwa kuwa kuna baadhi ya taarifa zinapatikana kupitia hati hiyo.
31	Chama kianzishe huduma ya *fixed account* itakayokuwa na riba inayovutia kwa ajili ya wastaafu kama inavyofanywa na benki ya NMB	Mbeya	Lipokelewa, Chama kinawakaribisha wanachama kuweka amana katika akaunti ya Fixed (Riba inayotolewa ni asilimia kati ya 3 hadi 5)
32	Chama kiharakishe mpango wa Wanachama wastaafu Kupitisha mafao yao kila mwezi	Ilala	Limepokelewa kwa utekelezaji katika mwaka wa fedha 2023

3.0 TAARIFA YA HESABU ZA CHAMA KUISHIA DISEMBA 2021

TAARIFA HURU YA MKAGUZI KWA WANACHAMA WA TANESCO SACCOS LTD

Ripoti inayohusu Taarifa za Fedha kwa mwaka ulioishia tarehe **31.12.2021**

Hati Inayoridhisha

Tumekagua taarifa za fedha za **TANESCO SACCOS Ltd**, ambazo zinajumuisha taarifa ya hali ya fedha ya tarehe 31 Disemba, 2021, na taarifa ya mapato na matumizi, taarifa ya mabadiliko ya mtaji na taarifa ya mtiririko wa fedha kwa mwaka ulioishia tarehe hiyo, na maelezo ya ufafanuzi wa taarifa za fedha, kujumuisha muhtasari wa sera muhimu za uhasibu.

Kwa maoni yetu, taarifa za fedha zilizoambatanishwa zinaonesha hali halisi ya fedha ya Chama cha Ushirika ya tarehe 31 Disemba, 2021, na matokeo ya shughuli zake pamoja na mtiririko wa fedha kwa mwaka ulioishia tarehe hiyo kulingana na matakwa ya Viwango vya Kimataifa vya Utoaji Taarifa za Fedha.

Msingi wa Maoni

Ukaguzi wetu ulifanyika kwa kuzingatia Viwango vya Ukaguzi vya Kimataifa. Wajibu wetu chini ya hivyo viwango umeelezwa katika aya ya wajibu wa mkaguzi kwa taarifa za fedha ya taarifa yetu. Tuko huru kulingana na matakwa ya maadili yanayohusiana na ukaguzi wetu wa taarifa za fedha Tanzania, na tumetimiza wajibu wetu mwingine wa maadili kulingana na matakwa haya. Tunaamini ushahidi wa ukaguzi ambao tumeupata unatosheleza na unafaa kwa ajili ya msingi wa hati inayoridhisha.

Mambo ya Msisitizo

1. Kiasi cha Tsh. 143,162,215 kinachoendelea kusuluhishwa

Tunatoa msisitizo katika jedwali Na. 16 la taarifa za fedha linalojumuisha kiasi cha Tsh. 143,162,215 kinachoendelea kusuluhishwa mjengeko wake. Kiasi hicho kinatokana na changamoto ya mfumo unaotumiwa na chama (Fin Financial toleo la 5) ya kutotambua baadhi ya maingizo ya miamala kwenye akaunti husika.

2. Kutozingatiwa kwa Uwiano wa Mtaji Toshelevu

Tunatoa msisitizo katika jedwali Na. 28 la taarifa hizi za fedha linaloonesha kwamba kunako tarehe 31 Disemba, 2021 uwiano wa mtaji Halisi 2.03% upo chini ya uwiano unaotakiwa wa 6% kama inavyoelekezwa na kanuni ya 18 ya Kanuni za Taasisi ndogo ndogo za fedha (Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo) za mwaka 2019.

Maoni yetu hayajabadilishwa kutokana na mambo haya.

Mambo Muhimu ya Ukaguzi

Mambo muhimu ya ukaguzi ni yale kwa ukadirifu wa taaluma yalikuwa muhimu zaidi katika ukaguzi wa taarifa za fedha za mwaka huu. Mambo haya yalielezwa katika muktadha wa ukaguzi wetu wa taarifa za fedha kwa ujumla, na katika kutoa maoni yetu juu yake, hatutoi maoni tofauti katika mambo haya.

Taarifa Nyingine

Uongozi wa Chama unawajibika kwa ajili ya taarifa nyingine. Taarifa nyingine ni pamoja na taarifa ya Wajumbe wa Bodi na Tamko la Mkuu wa Idara ya Fedha lakini hazijumuishi taarifa za fedha na taarifa yetu ya ukaguzi.

Maoni yetu juu ya taarifa za fedha hayahusishi taarifa nyingine na hatutoi uthibitisho wa aina yoyote juu yake. Ukiunganisha na ukaguzi wetu wa taarifa za fedha, wajibu wetu ni kusoma taarifa nyingine na kwa kufanya hivyo, tunaangalia kama taarifa nyingine kwa kiasi kikubwa haziendani na taarifa za fedha au uelewa wetu tulioupata wakati wa ukaguzi, ama vinginevyo zinaonekana kupotoshwa.

Iwapo, kutokana na kazi tuliyoifanya kuhusu taarifa nyingine itabainika kwamba kunaupotoshaji wa taarifa hizi nyingine, tunatakiwa kutoa taarifa juu ya ukweli huo. Hatuna jambo la kutolea taarifa kuhusu suala hili.

Wajibu wa Bodi ya Chama cha Ushirika

Bodi ya Chama cha Ushirika inawajibu wa kutayarisha na kuwasilisha taarifa hizi za fedha kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Utoaji Taarifa za Fedha pamoja na Sheria ya Vyama vya Ushirika Na.6 ya mwaka 2013. Vilevile bodi inawajibu wa kuweka mfumo wa udhibiti wa ndani ambao bodi inaona ni muhimu katika kutayarisha taarifa za fedha ambazo hazina dosari kubwa zinazotokana na udanganyifu au makosa ya kawaida.

Katika kutayarisha taarifa za fedha bodi inawajibu wa kutathmini uwezo wa Chama kuwa endelevu, ikionesha, kadri inavyofaa, mambo yanayohusiana na Chama kuwa endelevu na kutumia msingi wa uhasibu wa Chama kuwa endelevu isipokuwa ama bodi inakusudia kukifilisi Chama au kusitisha shughuli au hakina njia mbadala ya kweli isipokuwa kufanya hivyo.

Wajibu wa Mkaguzi

Shabaha yetu ni kupata uhakika wa maana kama taarifa za fedha kwa ujumla wake hazina upotoshaji mkubwa, ama kwa sababu ya udanganyifu au makosa ya kawaida, na kutoa taarifa ya mkaguzi ambayo inajumuisha maoni yetu. Uhakika wa maana ni kiwango cha juu cha uhakika, lakini siyo dhamana kwamba ukaguzi uliofanyika kulingana na viwango vya ukaguzi vya kimataifa kila mara utagundua upotoshaji mkubwa

unaokuwepo. Upotoshaji unaweza kutokana na udaganyifu au makosa ya kawaida na unafikiriwa kuwa mkubwa kama, peke yake au kwa ujumla, ungeweza kuathiri maamuzi ya watumiaji kwa msingi wa taarifa hizi za fedha.

Vilevile, kifungu cha 55(6) cha Sheria ya Vyama vya Ushirika Na.6 ya mwaka 2013 kinatutaka tujiridhishe kama shughuli za Chama cha Ushirika zimefanyika kulingana na matakwa ya Sheria au la na, kama vitabu na hesabu za Chama vina kubaliana na vinatoa hali halisi ya shughuli za Chama.

Kama sehemu ya ukaguzi kulingana na Viwango vya Ukaguzi vya Kimataifa, tunatumia maamuzi ya weledi na tunadumisha weledi wa kushuku wakati wote wa ukaguzi. Pia:

- Tunatambua na kutathmini hatari za upotoshaji mkubwa wa taarifa za fedha, ama kutokana na udanganyifu au makosa ya kawaida, kupanga na kufanya ukaguzi kuitikia hatari hizo, na kupata ushahidi unaotosheleza na kufaa kwa ajili ya msingi wa maoni yetu. Hatari ya kutogundua upotoshaji mkubwa unaotokana na udanganyifu ni kubwa kuliko hatari inayotokana na makosa ya kawaida, kwa sababu udanganyifu unaweza kuhusisha njama, kughushi, kuondoa taarifa kwa makusudi, mawasilisho yasiyo sahihi, au kupuuza mfumo wa udhibiti wa ndani.

- Kupata ufahamu wa udhibiti wa ndani kuhusiana na ukaguzi ili kupanga njia za ukaguzi ambazo zinafaa, lakini siyo kwa makusudi ya kutoa maoni juu ya kufaa kwa udhibiti wa ndani wa Chama.

• Kutathmini kufaa kwa sera za uhasibu zinazotumika na usahihi wa makadirio ya uhasibu na maelezo bayana yaliyofanywa na uongozi.

Kuhitimisha kufaa kwa matumizi ya bodi juu ya msingi wa uhasibu wa Chama kuwa endelevu na, kwa kuzingatia ushahidi wa ukaguzi uliopatikana, ama kuwepo kwa mashaka makubwa kuhusiana na matukio au hali inayoweza kuleta mashaka makubwa juu ya uwezo wa Chama kuendelea kuwa endelevu. Kama tunahitimisha kwamba yapo mashaka makubwa, tunatakiwa kuvuta nadhari katika taarifa yetu ya ukaguzi kuhusiana na maelezo bayana katika taarifa za fedha au, kama maelezo hayo hayatoshelezi, tubadilishe maoni yetu. Hitimisho letu limejengwa juu ya ushahidi wa ukaguzi tulioupata hadi kufikia tarehe ya taarifa yetu ya ukaguzi.

Hata hivyo, matukio au hali za siku za usoni zinaweza kusababisha Chama kukoma kuendelea kuwa endelevu.
Tunawasiliana na Bodi ya Chama cha Ushirika kuhusiana, miongoni mwa mambo mengine, mawanda yaliyopangwa na muda wa ukaguzi na matokeo makubwa ya ukaguzi, kujumuisha mapungufu yoyote makubwa katika udhibiti wa ndani ambayo tunayabaini wakati wa ukaguzi wetu.

Pia tunatoa taarifa kwa Bodi ya Chama cha Ushirika ya kwamba tumefuata matakwa ya miiko ya kuwa huru, na tunawasiliana nao kuhusu mahusiano na mambo mengine yote yanayoweza kufikiriwa kukiuka uhuru wetu na pale inapobidi jinsi ya kuulinda.

Ripoti Inayohusu Matakwa Mengine ya Kisheria na Usimamizi
Kulingana na matakwa ya kifungu cha 55(6) cha Sheria ya Vyama vya Ushirika Na.6 ya mwaka 2013, tunatoa taarifa kwa maoni yetu kwamba:

a) Vitabu vya hesabu vilivyotunzwa na Chama vinakubaliana na vinatoa hali halisi ya shughuli za Chama; na

b) Shughuli za Chama zimefanyika kulingana na madhumuni ya Chama, Masharti na maamuzi yaliyofanyika katika mkutano mkuu wa Chama.

SHIRIKA LA UKAGUZI NA USIMAMIZI WA VYAMA VYA USHIRIKA (COASCO)

CPA Z. E. MKINGULE
MKURUGENZI MKUU

Nakala: Mrajis wa Vyama vya Ushirika DODOMA
Mraji Msaidizi wa Vyama vya Ushirika (M) DAR ES SALAAM
Afisa Ushirika wa wilaya UBUNGO

TAARIFA YA HALI YA FEDHA MNAMO TAREHE 31.12.2021

RASILIMALI	JEDW	31.12.2021 TZS	31.12.2020 TZS
Taslimu na usawa	2	2,235,222,788	1,396,174,891
Mikopo ya wanachama	3	48,908,423,591	45,870,262,030
Wadaiwa	4	7,924,523,274	7,233,936,401
Uwekezaji	5	440,187,420	110,984,640
Mali za kudumu -zisizoshikika	6	480,983,662	363,980,587
Mali za kudumu- zinazoshikika	7	1,100,140,827	1,006,975,072
Kodi iliyoahirishwa	8	-	35,320,294
Kodi (Tax asset)	9	-	79,379,521
JUMLA YA RASILIMALI		**61,089,481,562**	**56,097,013,436**
MTAJI NA DHIMA			
Mtaji			
Akiba ya kukomboa mafungu		375,832,041	337,009,755
Akiba ya lazima		778,507,122	726,744,074
Akiba ya Elimu		383,965,831	358,084,307
Akiba ya madeni mabaya		95,444,347	56,622,061
Akiba ya kukuza Mtaji		257,046,981	231,165,457
Limbikizo la uwekezaji		71,299,780	42,097,000
Limbikizo la zida		447,264,870	369,620,299
Uthamanishaji wa mali za kudumu		26,002,272	26,002,272
Jumla ya Mtaji		**2,435,363,243**	**2,147,345,224**
Dhima			
Hisa za wanachama	10	9,462,104,242	8,526,164,766
Akiba za wanachama	11	41,959,533,244	39,879,206,954
Amana za wanachama	12	1,491,868,011	1,437,267,090
Wadai wa riba ya akiba na hisa	13	733,866,458	-
Mfuko wa rambi rambi	14	634,177,927	575,932,311
Mfuko wa kuijali Jamii (CSR)	15	15,000,000	15,000,000
Wadai wengine	16	1,594,545,341	1,206,959,468
Mfuko wa Tahadhari	17	2,634,714,862	2,211,866,576
Tengo la kodi ya zuio	18	81,540,717	97,271,046
Tengo la kodi ya mapato	9	45,358,284	-
Kodi iliyoahirishwa	8	1,409,233	-
Jumla ya Dhima		**58,654,118,319**	**53,949,668,211**
JUMLA YA DHIMA NA MTAJI		**61,089,481,562**	**56,097,013,435**

JEDWALI NAMBA 1 HADI 35 NI SEHEMU YA HESABU HIZI

.....
MWENYEKITI

TAREHE: ..... 25/07/2022 .....

.....
MENEJA

TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KUISHIA TAREHE 31.12.2021

		MWAKA 2021	MWAKA 2020
MAPATO		**TZS**	**TZS**
Faida juu ya mikopo	19	4,741,755,593	4,181,143,397
Gharama za riba	20	(815,407,176)	(972,710,465)
Baki ya faida juu ya mikopo		3,926,348,418	3,208,432,932
Mapato ya FOSA	21	181,764,360	182,947,020
Mapato mengineyo	22	58,796,539	158,848,316
Jumla ya mapato		**4,166,909,316**	**3,578,320,117**
MATUMIZI			
Gharama za utumishi	23	886,196,046	738,330,663
Gharama za utawala	24	641,324,105	341,198,568
Gharama za uendeshaji	25	642,530,104	829,102,588
Gharama za biashara	26	334,701,467	373,146,489
Gharama za mkutano mkuu	27	1,204,062,550	1,107,063,601
Jumla ya Matumizi		**3,708,814,272**	**3,388,841,909**
Ziada kabla ya tengo la kodi		458,095,044	161,386,358
Kodi ya mapato	28	(199,279,806)	(150,233,487)
Ziada ya mwaka baada ya kodi		**258,815,239**	**11,152,872**
Mapato mengineyo ya kina (OCI)			
Ongezeko la thamani hisa za CRDB na DSE	5	29,202,780	26,612,400
Jumla ya mapato ya kina		**288,018,019**	**37,765,272**

JEDWALI NAMBA 1 HADI 35 NI SEHEMU YA HESABU HIZI

.....

MWENYEKITI

TAREHE: **25/07/2022**

.....

MENEJA

TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA MWAKA ULIOISHIA TAREHE 31.12.2021

MAELEZO	AKIBA YA LAZIMA	AKIBA YA KUKOMBOA MAFUNGU	AKIBA YA ELIMU	AKIBA YA MADENI MABAYA	AKIBA YA KUKUZA MTAJI	LIMBIKIZO LA ZIADA	LIMBIKIZO LA UTHAMIN ISHAJI	JUMLA
	TZS	**TZS**	**TZS**	**TZS**	**TZS**	**TZS**	**TZS**	**TZS**
	20%	15%	10%	15%	10%			-
Salio kunako 1.01.2020	**724,513,500**	**335,336,824**	**356,969,020**	**54,949,130**	**230,050,170**	**192,016,773**	**26,002,272**	**1,936,889,488**
Mabadiliko							-	25,045,200
Bonus ya wafanyakazi						(17,858,112)		(17,858,112)
Msamaha wa kodi kutoka nyuma (Jed Na. 32)						192,115,776		192,115,776
Ziada ya mwaka						11,152,872		11,152,872
Matengo ya mwaka	2,230,574	1,672,931	1,115,287	1,672,931	1,115,287	(7,807,010)		-
Baki Kunako 31.12.2020	**726,744,074**	**337,009,755**	**358,084,307**	**56,622,061**	**231,165,457**	**369,620,299**	**26,002,272**	**2,147,345,224**
Salio kunako 1.01.2021	**726,744,074**	**337,009,755**	**358,084,307**	**56,622,061**	**231,165,457**	**369,620,299**	**26,002,272**	**2,147,345,224**
Mabadiliko ya thamani ya hisa							-	29,202,780
Bonus ya wafanyakazi								-
Madadiliko ya nyuma						-		-
Ziada ya mwaka						258,815,239		258,815,239
Matengo ya mwaka	51,763,048	38,822,286	25,881,524	38,822,286	25,881,524	(181,170,667)		-
Baki Kunako 31.12.2021	**778,507,122**	**375,832,041**	**383,965,831**	**95,444,347**	**257,046,981**	**447,264,870**	**26,002,272**	**2,435,363,243**

JEDWALI NA 1 HADI 35 NI SEHEMU YA HESABU HIZI

.....
MWENYEKITI

TAREHE: **25/07/2022**

.....
MENEJA

TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA MWAKA ULIOISHIA TAREHE 31.12.2021

	31.12.2021 TZS	31.12.2020 TZS
MTIRIRIKO WA FEDHA TOKA UENDESHAJI		
Ziada kabla ya tengo la kodi	458,095,044	161,386,358
Masahisho ya:		
- Uchakavu wa mali na vifaa	194,992,454	131,479,172
- Mabadiliko ya Thamani ya hisa wekezwa	-	4,706,400
- Ongezeko la karisaji	122,280,569	314,728,212
- Riba ya mawekezo CRDB	(13,929,295)	(17,849,496)
Mtiririko kabla ya mabadiliko ya mtaji	**761,438,773**	**594,450,646**
(Kuongezeka)/kupungua Mikopo ya Wanachama	(3,160,442,130)	(7,597,036,745)
(Kuongezeka)/kupungua Wadaiwa-wengine	(690,586,873)	3,000,964,960
Kuongezeka/(kupungua) hisa	935,939,476	1,149,588,698
Kuongezeka/(kupungua) Akiba za Wanachama	2,080,326,290	2,797,735,717
Kuongezeka/(kupungua) Amana za wanachama	54,600,921	(204,931,978)
Kuongezeka/(kupungua) mfuko wa rambirambi	58,245,616	131,655,617
Kuongezeka/(kupungua) mfuko wa Tahadhari	422,848,286	451,965,542
Kuongezeka/(kupungua) wadai wengine	387,585,873	66,869,269
Kuongezeka/(Kupungua) kodi za serikali	(15,730,329)	11,088,654
Kuongezeka/(kupungua) wadai wa riba ya akiba na hisa	733,866,458	(142,135,609)
Mtiririko kutoka shughuli za Uendeshaji	**806,653,587**	**(334,235,873)**
Kodi iliyolipwa TRA	(37,812,474)	(205,288,782)
Fedha halisi toka/(tumika) Uendeshaji	**1,530,279,887**	**54,925,990**
MTIRIRIKO WA FEDHA TOKA UWEKEZAJI		
Ongezeko la Mali za Kudumu	(405,161,285)	(380,693,160)
Riba ya mawekezo CRDB	13,929,295	17,849,496
Mawekezo ya FDR	(300,000,000)	
Fedha halisi tumika shughuli za uwekezaji	**(691,231,990)**	**(362,843,664)**
MTIRIRIKO WA FEDHA TOKA SHUGHULI ZA FEDHA		
Staff bonus	-	(17,858,112)
Fedha halisi tumika shughuli za fedha	-	(17,858,112)
	839,047,897	(325,775,785)
Fedha mwanzoni 01.01.2021	1,396,174,891	1,721,950,676
Fedha mwishoni 31.12.2021	**2,235,222,788**	**1,396,174,891**

JEDWALI NAMBA 1 HADI 35 NI SEHEMU YA HESABU HIZI

.....

MWENYEKITI

TAREHE: **25/07/2022**

.....

MENEJA

3.0 MAAZIMIO YA MKUTANO MKUU 2022

i. Mkutano Mkuu umeidhinisha ukomo wa madeni wa kiasi cha Tshs. Bilioni 5 kwa ajili ya kuongeza ukwasi na utoaji wa mikopo.

ii. Mkutano Mkuu umeridhia kuongeza viwango vya uchangiaji kwa akiba na hisa kama ifuatavyo

	Akiba	Hisa
Mwanachama	55,000-100,000	10,000-20,000
Wawakilishi	55,000-200,000	15,000-20,000
Viongozi wa Bodi na Kamati ya usimamizi	100,000-300,000	15,000-50,000

iii. Mkutano Mkuu umeridhia kusitisha upunguzaji wa akiba kuanzia sasa ili kuongeza ukwasi na kukuza mtaji wa Chama.

iv. Mkutano Mkuu kuratibu maandalizi ya Mpango Mkakati mpya wa Chama kwa mwaka 2024 - 2028.

v. Mkutano Mkuu umeazimia kwa mwaka 2023 kuhuishwa kwa masharti ya Chama na sera mbalimbali ili kuakisi mazingira ya biashara na hatari zinazoweza kusababisha hasara katika Chama.

vi. Mkutano Mkuu umepitisha Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (COASCO) kuwa Mkaguzi wa Hesabu za Chama kwa kipindi kinachoishia tarehe 31 Disemba 2022.

vii. Mkutano Mkuu umeridhia uchaguzi wa wawakilishi matawini kwa mwaka 2023 ufanyike katika mikutano ya mrejesho wa Mkutano Mkuu wa mwaka 2022 ili kuwezesha uratibu wa semina ya wawakilishi.

viii. Mkutano Mkuu umeridhia ujenzi wa jengo la ofisi ya Chama katika kiwanja cha Mwenge utaanza mwaka 2024 baada ya ukwasi na hali ya utoaji huduma kuimarika.

ix. Mkutano Mkuu umeridhia ili Mwanachama aweze kugombea nafasi ya uwakilishi atapaswa kuwa na akiba zisizopungua Tshs. Milioni 10 na viongozi wa Bodi na kamati ya usimamizi kuwa na akiba ya Tshs. Milioni 20.

4.0 TAARIFA KUHUSU HUDUMA ZA MIKOPO NA CHANGAMOTO ZA UKWASI

Uongozi wa Chama unawajulisha wanachama tangu mwezi Agosti 2022 Chama kimekumbwa na changamoto ya ukwasi unaojitosheleza kuweza kulipa maombi ya mikopo kwa wakati kwa wanachama wanakidhi vigezo.

Hali hii imesababishwa na kuimarika kwa uwezo wa wanachama kukopesheka (fursa kwa Chama kukuza mizania na kutanua huduma). Lakini pia fursa hii imekutana uchache wa ukwasi uliopo ndani ya Chama wakati huo.

Pamoja na changamoto hii kuwa bado inaendelea, Uongozi wa Chama unapenda kuwaelewesha wanachama yafuatayo kuhusu suala hili:

1. Chama kina wanachama wapatao 6,354 kuishia Disemba 2022 wanaomiliki jumla ya hisa na akiba Tshs. 54,491,841,000 na wakiwa na mikopo jumla ya Tshs. 59,585,444,000. Hivyo basi, Chama bado kiko mara kwa maana bado kinaendelea kuwakopesha kwa kutumia vyanzo vya ndani vya hisa na mikopo.

2. Kuimarika kwa wigo wa wanachama kukopesheka, kunaweza kuchukuliwa kwenye mtizamo ufuatao;

   Case 1: Kama wanachama zaidi ya 4,000 wakiwa wameongezewa uwezo na Mwajiri wa kukopesheka, lakini wakati huo huo, hawajaongeza HISA na AKIBA zao kwa kiwango cha kutosha, Chama hakiwezi kuwa na uwezo wa kuwapoesha wote kwa wakati mmoja.

   Case 2: Kama kiwango walichoongezewa wanachama 4,000 kukuza uwezo wao wa kukopesheka, Kama Mwajiri angekuwa ameajiri wafanyakazi wapya 4,000 na kuwalipa hilo ongezeko, na kwa wakati mmoja wafanyakazi hao wapya wakawa wanachama wa TANESCO SACCOS, na wakataka mikopo kwa wakati mmoja, Chama kisingeweza kuwakopesha wote kwa wakati mmoja, kwani HISA na AKIBA zao zisingetosheleza.

   Hivyo basi vyovyote vile, Chama kinahitaji wanachama waendelee kuchangia HISA na AKIBA na baada ya muda uwezo wa kuwakopesha wanachama utaongezeka na tutarudi katika hali ya kawaida.

3. Licha ya hali hii, huduma za mikopo zimeendelea kwa utaratibu wa fomu ya kwanza kupokelewa ina kuwa ya kwanza kuhudumiwa (FIFO), na taarifa ya mikopo iliyotolewa katika kipindi ni kama inavyooneshwa katika jedwali hapa chini:

Kipindi-2022	Mkopo	Wanachama	Kiasi (Tshs)
Agosti	Maendeleo	160	2,237,033,004.29
Septemba	Maendeleo	314	4,438,728,117.02
Agosti	B/Maisha	105	1,747,915,337.31
Septemba	B/Maisha	152	2,817,247,302.27
	Jumla	**731**	**11,240,923,760.89**

Tanbihi: Mikopo mengine yote inalipwa kama kawaida

4. Uongozi wa Chama umechukua hatua kadhaa ili kupata suluhisho la hali hii, na hatua zilizochukuliwa ni pamoja na
   - Kuwajulisha wanachama kupitia Mkutano Mkuu uhumihu na ulazima wa kuongeza kiwango cha uchangiaji wa hisa na akiba, na kupata maamuzi ya Mkutano Mkuu ya kupandisha viwango hivyo kupitia waraka Na. TS/WARAKA/2022/02 wa tarehe 12.11.2022 (Umejumuishwa katika kijarida hiki)

   - Kuomba mkopo wenye riba nafuu kutoka kwa benki wadau kiasi cha Tshs. 4,000,000,000 ili kupunguza foleni ya maombi ya mikopo ya wanachama iliyopo. Mtarajaio ni kupata mkopo huo ndani ya mwezi Machi 2023.

CHAMA CHA USHIRIKA WA AKIBA NA MIKOPO TANESCO

KUTOKA: MWENYEKITI **Kumb. Na. TS/WARAKA/2022/02**	**KWENDA: WANACHAMA WOTE** **TAREHE: 12.11.2022**

YAH: HUDUMA NA UKWASI KATIKA CHAMA NA UCHAGUZI 2023

Rejea somo lililotajwa hapo juu.

Uongozi wa Chama unapenda kuwajulisha kuwa kipindi cha hivi karibuni, kuanzia mwezi Agosti 2022, Ofisi ya Chama imepokea maombi mengi ya mikopo yaliyosababishwa na kuimarika kwa wigo wa kukopesheka kwa wanachama kufuatia maboresho yaliyofanywa na Mwajiri.

Ongezeko hili la maombi ya mikopo, limesababisha changamoto ya ukwasi katika Chama hasa ikizingatiwa kuwa makusanyo ya mwezi hayatoshelezi kukidhi maombi yaliyowasilishwa. Hivyo kusababisha malipo kufanyika kwa utaratibu wa kwanza kupokelewa fomu, wa kwanza kulipwa (FIFO). Hali hii imezalisha malalamiko na kukwama kwa mipango na matarajio ya wanachama katika juhudi za kujiletea maendeleo kupitia mikopo nafuu inayotolewa na Chama.

Chama ni cha wanachama, Kupitia Mkutano Mkuu wa mwaka 2022, uliofanyika tarehe 22 na 23 Oktoba 2022, Dar es salaam wawakilishi kwa pamoja walipitisha maazimio ya utekelezaji kwa kuchukua hatua za haraka za muda mfupi na mrefu ili kukabiliana na changamoto hii ya ukwasi. Maazimio hayo ni kama ifuatavyo;

Moja, Uongozi kuratibu upatikanaji wa mkopo kutoka taasisi wadau kwa masharti nafuu ya riba ili kuwezesha malipo ya mikopo, pasi kuathiri viwango vya riba zinazotozwa kwa sasa na Chama.

Pili, Kusitisha huduma za kupunguza akiba za lazima kuanzia tarehe 23 Oktoba 2022 na kufanya maboresho ya sera ya akiba, amana na gawio ili kukuza uwezo wa ndani wa kutoa mikopo.

Tatu, Kupandisha viwango vya uchangiaji wa akiba na hisa kwa mwezi kwa makundi ndani ya Chama, kuanzaia tarehe 01 Novemba 2022.

Kundi	Akiba (Tshs.)	Hisa (Tshs.)
Mwanachama	55,000-100,000	10,000 -20,000
Wawakilishi	55,000-200,000	15,000 -20,000
Viongozi Bodi na Kamati-U	100,000-300,000	15,000 -50,000

Nne, Kuboreshwa kwa vigezo vya kukidhi sifa kwa viongozi wa Chama katika makundi tofauti kwenye uchaguzi wa mwaka 2023 ndani ya Chama, Kigezo kilichoboreshwa ni kuwa na kiwango cha chini cha akiba kama inavyoonekana katika jedwali:

Kundi	Akiba (Tshs.)
Wawakilishi	10,000,000 au zaidi
Viongozi Bodi na Kamati-U	20,000,000 au zaidi

Tanbihi:

i. Uchaguzi kwa wawakilishi kwa mwaka 2023, utafanyika katika Mikutano ya Mrejesho itakayofanyika kati ya mwezi Februari na Aprili 2023

ii. Uchaguzi wa viongozi wa Bodi na Kamati ya Usimamizi utafanyika kati ya mwezi Oktoba na Novemba 2023

iii. Kwa upande wa wawakilishi, Mwanachama anaweza kuchaguliwa hata kama hatakuwa ametimiza akiba ya Tshs. 10,000,000 wakati wa zoezi la Uchaguzi, lakini atapewa muda wa mpito kukamilisha kigezo hicho kabla ya kufanyika Mkutano Mkuu wa mwaka 2023.

iv. Hivyo, kila Mwakilishi wa tawi la TANESCO SACCOS atapaswa kuwa na akiba ya zisizopungua Tshs. 10,000,000 wakati wa Mkutano Mkuu 2023.

v. Waraka huu umetolewa, ili kuwaarifu wanachama hatua zinazochukuliwa na Uongozi kurudisha hali ya utoaji huduma ndani ya Chama chetu na kuwandaa viongozi watarajiwa juu ya masharti na vigezo vipya vilivyoongezwa.

Pamoja na Salaam za Ushirika.

Somoe I. Nguhwe
Mwenyekiti
TAARIFA ZA MARUDIO

HUDUMA ZA MIKOPO – MAKUNDI YA WASTAAFU NA WENZA.

Chama katika mkakati wa kuendelea kukuza mizania na kutanua wigo wa huduma kinatarajia kufanya maboresho kadhaa kwa huduma za mikopo kwa makundi ya wastaafu na wanachama wenza.

WANACHAMA KUNDI LA WASTAAFU

Chama kinatarajiwa kuunganisha mifumo ile ya TANESCO SACCOS na Benki ya TCB na Mfuko wa hifadhi wa jamii kwa watumishi wa umma (PSSSF) na kuwezesha uchakataji wa Pensheni za wastaafu kupitia TANESCO SACCOS, Suala hili litatatekelezwa ndani ya mwaka huu 2023 baada ya kuidhinishwa na Mrajis.

Hatua hii ni kubwa na mafanikio sana kwa Chama na wanachama kwa kuwa:

- Chama kitaweza kukuza ukwasi kwa kupitisha pensheni za mkupuo na mwezi za wastaafu.
- Dhana ya uanachama wa kudumu sasa itatekelezeka kwa ufanisi zaidi.
- Wanachama watakuwa hawana hofu ya kukopa mikopo wakihofia kukaribia kwa muda wao wa kustaafu. Hii itawezesha kuchukua mikopo mikubwa na kufanya maandalizi ya awali ya kustaafu.
- Wastaafu wataweza kukopa kama Mwanachama mwingine na kulipa mkopo kwa pensheni ya kila mwezi.

WANACHAMA KUNDI LA WENZA

Kundi hili ni maalum, hasa kwa kigezo cha kuwa na mdhamini mkuu ***(principal Guarantor)*** ni mwenza wa mwanachama mwenyewe. Mwanachama wa kundi hili atadhaminiwa mikopo yote na mwenza wake wakati wote.

MIKOPO YA BOSA

Mkopo/Mara	Maendeleo	Dharura	Elimu
Mara 1	200% (Mwanachama ataruhusiwa kukopa mpaka mara 2 ya akiba zake)	<1m (Mwanachama ataruhusiwa kukopa mpaka kiasi kisichozidi Tshs. 1,000,000 zake)	X1 Mshahara (Mwanachama ataruhusiwa kukopa mpaka mara 1 ya Mshahara wake)
Mara 2+	300%(Mwanachama ataruhusiwa kukopa mpaka mara 3 ya akiba zake)	<2m(Mwanachama ataruhusiwa kukopa mpaka kiasi kisichozidi Tshs. 2,000,000 zake)	X3 Mshahara (Mwanachama ataruhusiwa kukopa mpaka mara 2 ya Mshahara wake)
Mara 3+	400%(Mwanachama ataruhusiwa kukopa mpaka mara 4 ya akiba zake)	<3m (Mwanachama ataruhusiwa kukopa mpaka kiasi kisichozidi Tshs. 3,000,000 zake)	X3 Mshahara (Mwanachama ataruhusiwa kukopa mpaka mara 2 ya Mshahara wake)

MIKOPO YA FOSA

Mkopo/Mara	Boresha	Usafiri	Wekeza	Likizo	Ujasiriamali
Mara 1	300% (Mwanachama ataruhusiwa kukopa mpaka mara 3 ya mshahara wake)	<15m ((Mwanachama ataruhusiwa kukopa gari lisilozidi milioni 15)	x2 Hisa za Hiyari	x2 Amana	<10m
Mara 2+	400% Mshahara (Mwanacha-ma ataruhusiwa kukopa mpaka mara 4 ya mshahara wake)	<20m (Mwanachama ataruhusiwa kukopa gari lisilozidi milioni 20)	x2 Hisa za Hiyari	x2 Amana	<10m
Mara 3+	500% Mshahara (Mwanacha-ma ataruhusiwa kukopa mpaka mara 5 ya mshahara wake)	<25m (Mwanachama ataruhusiwa kukopa gari lisilozidi milioni 25)	x2 Hisa za Hiyari	x2 Amana	<10m

Tanbihi:
Makundi ya wastaafu, wenza na wanachama amabo ni Watoto wa Wananchama (Principal) wataruhusiwa kuchangia kiwango cha akiba kuanzia Tshs. 55,000+ nah isa Tshs. 10,000+ ili kuweza kuwahudumia kulingana na umaalumu wao.

MKOPO WA BORESHA MAISHA

- Mwanachama ana uhuru wa kukopa kiwango huru kinachokatika mpaka mara 60
- Riba ya mkopo huu itakuwa asilimia 1.0 kwa mwezi kwa baki ya mkopo
- Kiwango cha juu cha mkopo kitakuwa Tshs. milioni thelathini
- Muda wa juu wa marejesho ya mkopo ni miezi sitini (60)
- Mwanachama ataruhusiwa kukopa tena iwapo atakuwa amemaliza mkopo wa awali, au amerejesha nusu (1/2) ya deni la awali
- Mkopo huu utaweza kununua madeni ya taasisi nyingine za fedha
- Mkopo huu kutolewa kila siku (Hausubiri kikao cha Kamati)

MKOPO WA UJASIRIAMALI

- Mwanachama anaweza kukopa kiwango kisichozidi Tshs. 10,000,000
- Riba ya mkopo huu itakuwa asilimia 1.375 kwa mwezi kiasi cha mkopo
- Muda wa juu wa marejesho ya mkopo ni miezi ishirini na nne (24)
- Mwanachama atatakiwa kuwasilisha: Mpango wa biashara (lazima), leseni ya biashara, usajili wa biashara (business name) na namba ya utambulisho wa mlipa kodi (kama biashara hiyo imesajiliwa)
- Mwanachama lazima apitishe Mshahara FOSA, Dhamana za mkopo huu zimefutwa ili kuwarahishia wanachama kuanzisha na kukuza biashara zao.

MKOPO WA PAPO KWA PAPO

- Utatolewa kwa kiwango cha kuanzia Tshs. 50,000.00 hadi Tshs. 300,000.00 kuanzia tarehe 10 hadi 20 ya kila mwezi.
- Makato ya marejesho ya mkopo huu yatafanyika mwezi unaofuata kwa mkupuo mmoja.
- Riba ya mkopo wa papo kwa hapo ni asilimia 08

MKOPO WA USAFIRI

Mwanachama anaweza ku-top up mkopo wa gari baada ya kulipa nusu ya thamamni ya mkopo wa awali kwa kuagiza gari jingine.

- Mwanachama anaweza kukopa chombo cha usafiri kupitia mawakala wa Be Forward au SBT Tanzania.
- Kiwango cha mkopo kisichozidi shilingi milioni hamsini (Tshs. 50,000,000).
- Riba ya mkopo huu itakuwa asilimia 9.6 kwa mwaka (reducing balance).
- Marejesho ya mkopo huu yatafanyika ndani ya miezi arobaini na nane (48).
- Marejesho ya Mkopo huu yatafanyika kupitia Akaunti yake ya FOSA.
- Chama kitashikilia hati halisi ya umiliki wa gari mpaka Mwanachama atakapo maliza deni.
- Kwa Mwanachama aliye top-up, Chama kitashikilia hati halisi ya umiliki wa gari zote mbili, mpaka Mkopo utakapofika nusu, Ndio anaweza kuruhurusiwa kuchukua hati moja (ya gari la kwanza).
- Hati hizi itakuwa dhamana ya Mkopo huu. Kwa kipindi chote cha mkopo huu, ma/gari litakatiwa bima kubwa.

BIMA YA GARI

- Mwanachama anaweza kuomba mkopo wa bima ya gari kulingana na thamani ya gari yake.
- Bima hii inaweza kuwa bima kubwa (comprehensive) au bima ndogo (third party)
- Riba kwa mikopo ya Bima ya gari itakuwa asilimia 2 kwa mwezi kwa baki ya mkopo.
- Marejesho ya mkopo huu yatafanyika ndani ya muda wa miezi kumi na mbili (12)
- Chama kinashirikiana na Kampuni ya Jubilee Insurance (Tanzania).

MKOPO WA CHIPUKIZI

- Mkopo huu utatolewa kwa Mwanachama ambaye ameajiriwa ndani ya kipindi cha miezi 12
- Riba ya mkopo huu itakuwa asilimia 1.3 kwa mwezi kwa baki ya mkopo
- Mwanachama anaweza kukopa kiwango ambacho hakizidi mara tano (5) ya mshahara halisi wa mwezi.
- Muda wa juu wa marejesho ya mkopo ni miezi ishirini na nne (24) kwa wafanyakazi wa kudumu na miezi kumi na mbili (12) kwa wafanyakazi wa mkataba wa muda maalum.

MKOPO WA WEKEZA

- Mwanachama anaweza kukopa mpaka mara mbili (2) ya kiasi cha hisa za hiyari.
- Riba ya mkopo huu itakuwa asilimia 8 kwa mwaka (flat rate).
- Mwanachama ataruhusiwa kukopa tena iwapo atakuwa amemaliza mkopo wa awali.
- Marejesho ya mkopo huu yatafanyika ndani ya miezi kumi na mbili (12).
- Marejesho ya Mkopo huu yatafanyika kupitia Akaunti yake ya FOSA.

MKOPO YA MAENDELEO

- Mwanachama ana uhuru wa kukopa kiwango ambacho hakizidi mara nne (4) ya akiba.
- Mwanachama ataruhusiwa kukopa tena iwapo atakuwa amemaliza mkopo wa awali, au amerejesha moja ya tatu (1/3) la deni la awali.
- Riba kwa mkopo wa maendeleo ni asilimia 1.0 kwa mwezi kwa baki ya mkopo
- Muda wa juu wa marejesho ya mkopo ni miezi sitini (60)

MKOPO WA DHARURA

- Mkopo huu utatolewa kwa wanachama kwa kisichozidi Tshs. 3,000,000.00.
- Mkopo wa dharura hautatolewa kwa mwanachama ambae atakuwa bado hajamaliza mkopo wa awali.
- Riba kwa mikopo ya dharura itakuwa asilimia 2 kwa mwezi kwa baki ya mkopo.

MKOPO WA ELIMU

- Kiwango cha mkopo wa Elimu hakitazidi mara tatu ya mshahara wa mwanachama.
- Riba ya mkopo wa Elimu ni asilimia tano (5% flat rate) ya kiwango cha mkopo.
- Makato kwa mkopo wa Elimu yatafanyika kwa kipindi kisichozidi miezi kumi na mbili.

MKOPO WA LIKIZO (FOSA FESTIVAL LOAN)

- Mwanachama anaweza kukopa mara mbili (2) ya amana ya Likizo.
- Riba ya mkopo huu itakuwa asilimia 8 kwa mwaka (flat rate).
- Marejesho ya mkopo huu yatafanyika ndani ya muda wa miezi kumi na mbili (12)
- Marejesho ya Mkopo huu yatafanyika kupitia Akaunti yake ya FOSA.

AKAUNTI ZA AMANA -

Akaunti ya Kido, kwa ajili ya watoto wa wanachama walio na umri chini ya miaka 18

UTARATIBU WA KUFUNGUA AKAUNTI YA KIDO

Mwanachama (Mzazi/Mlezi) atapakua fomu kutoka Katina tovuti na kuijaza kikamilifu na kutuma ofisi za Chama. Akaunti hii itakuwa na vigezo vifuatavyo;

- Kiwango cha chini cha fedha katika zao hili la amana ni Tsh. 20,000
- Kiwango cha chini cha kuwekeza kila mwezi ni Tsh. 20,000
- Hakuna gharama za uendeshaji wa akaunti hii (no ledger fee or withdraw fee)
- Kutoa fedha inaruhusiwa mara 2 kwa mwaka
- Akaunti itasimamiwa na Mzazi/Mlezi hadi pale mtoto atakapofikisha umri wa 18
- Mwanachama anaweza kuweka standing order kupitia akaunti yake ya FOSA

UTARATIBU WA KUHAMISHA MSHAHARA FOSA

Uongozi wa Chama unawahamisisha Wanachama kutumia huduma za FOSA kwa kupitisha mshahara wa mwezi ili Mwanchama aweze kufaidi wigo mpana wa bidhaa zilizoboreshwa. Kwa kuzingatia changamoto zilizopo za Wanachama kufanikisha mchakato wa kuhamisha akaunti ya kupitisha mshahara kutoka ile ya benki kuja FOSA, Uongozi unawajulisha wanachama juu ya hatua mahsusi za kuchukua.

- Mwanachama kufuatilia na barua ya hali (status) madeni katika akaunti husika, Hapa hata kama unadeni katika benki hiyo Chama kitalinunua deni hilo baada ya kupokea barua rasmi ya benki na Mwanachama kujaza fomu ya mkopo wa Boresha kutaka deni hilo linunuliwe. Mchakato wa kupitia kwa Mwajiri kujua hali ya madeni pia utaendelea kutumia kwa msaada ya maafisa utumishi wa Mikoa/ Wilaya.
- Baada ya deni kununuliwa Chama kitampatia Mwanachama risiti ya uthibitisho wa kulipwa kwa deni, ambayo Mwanachama ataiwasilisha benki, KUWATAKA kutoa taarifa (status) kuwa HANA DENI, na kisha kufanikiwa kuhamisha mshahara FOSA. Hatua hii imeboreshwa ili kuwarahisishia wanachama wenye madeni chini ya Tshs. 15,000,000/= kuweza kuhamia FOSA.
- Barua ya hali (status- haudaiwi) kutoka benki itaambatanishwa na barua (inapatikana kwenye tovuti) na kuwasilishwa aidha ofisi za Chama au kwa Mwajiri moja kwa moja.

KUSAJILI WANACHAMA KATIKA MFUMO WA FOSA MOBILE

Uongozi wa Chama unawahamasisha wanachama wajisajili katika mfumo wa FOSA mobile ili kuweza kujihudumia baadhi ya huduma wakati wowote, kwa urahisi na uhakika.

Namna ya kujisajili, fuata hatua zifuatazo;

1. Pakua Application kutoka katika PLAYSTORE
2. Jisajili kwa kuweka taarifa zako kwa kadri mtiririko unavyokutaka
3. Akaunti namba yako wa FOSA utaweka **10100100 * * * * 310100** (Tarakimu nne ni kama zilizo katika kadi yako ya FOSA Mfano **L101- 001/00 * * * * - 00)**
4. Kipengele za mwaka wa kuzaliwa: Tafadhali bofya sehemu ya mwaka ili kupata mtiririko wa miaka ya nyuma kwa urahisi.
5. Baada ya kumaliza kujaza taarifa zote, utapokea Nywila (Password) ya kuanzia kupitia ujumbe mfupi, weka nywila hiyo na kubadili UNAYOTAKA KUWA NAMBA YAKO YA SIRI.

Nb: Kwa changamoto za taarifa kutofautiana afisa wa Chama atakupatia fomu maalum ya kubadili taarifa zako.

KUSAJILI WANACHAMA KATIKA MFUMO WA FOSA MOBILE- USSD

Uongozi wa Chama unawahamasisha wanachama wajisajili katika mfumo wa FOSA mobile kwa wanachama wasiokuwa na simu JANJA ili kuweza kujihudumia baadhi ya huduma wakati wowote, kwa urahisi na uhakika.

Namna ya kujisajili, fuata hatua zifuatazo;

1. Piga code yetu namba *150*59#
2. Changua namba 2 : Jisajili
3. Utajaza majibu ya maswali kwa kadri unavyoulizwa
4. Kwenye kitambulisho: Weka kampuni namba mfano X06666
5. Akaunti namba yako wa FOSA utaweka 10100100 * * * * 310100 (Tarakimu nne ni kama zilizo katika kadi yako ya FOSA Mfano L101- 001/00 * * * * - 00)
6. Endelea kujibu maswali mpaka mwisho.

Nb: Kwa changamoto za taarifa kutofautiana afisa wa Chama atakupatia fomu maalum ya kubadili taarifa zako

AHADI YA MWANACHAMA WA TANESCO SACCOS

Ahadi hii inawekwa na Mwanachama wa Chama cha Ushirika wa akiba na mikopo TANESCO kwa lengo la kuinua, kulinda, na kujivunia kuwa Mwanachama wa TANESCO SACCOS. Mwanachama wa TANESCO SACCOS kwa wakati wote atapaswa/anapaswa:

i. Kufahamu na kujishughulisha kufahamu taratibu mbalimbali zinazoendesha Chama kwa nia ya kuzifuata na kuziboresha inapobidi.

ii. Kukitetea Chama mara zote pale taswira ya Chama inapotaka kuharibiwa na mtu yeyote.

iii. Kulinda na kujuvunia kuwa Mwanachama wa TANESCO SACCOS kwa kuamini yeye ni mmiliki na mteja kwa wakati mmoja, hakuna mmiliki, mteja au mtetezi mwingine.

iv. Kuheshimu taratibu, viongozi, wanachama na wafanyakazi wa Chama kwa lengo la kuruhusu ustawi wa mihimili mitatu tegemezi ya Uongozi, Wanachama na Wafayakazi ili kuleta tija.

v. Kushauri /kupendekeza/ kukosoa kupitia Mikutano rasmi, lugha za staha ili kupata matokea chanya.

vi. Kukipenda Chama kwa dhahiri, kwa kuwa NDIO CHETU, hatuna kingine.

Ubungo Business Park,
S.L.P. 54231 Dar es Salaam

Simu 1: +255 733 140 107,
Simu 2: +255 737 584 782

info.saccos@tanescosaccos.or.tz

Tanesco Saccos LTD.

@tanescosaccos

www.tanescosaccos.or.tz